JUMUIYA YA TAWALA ZA MITAA TANZANIA

(ALAT)

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC)

UZOEFU KUTOKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA

MRADI WA UBORESHAJI WA SOKO LA MBOGAMBOGA NA MATUNDA, KIBAIGWA

Uzoefu Kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa

Mkoa wa Dodoma-Tanzania

Ripoti ya Mradi Imeandaliwa
na

Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT)
S.L.P. 2049
DODOMA

Imefadhiliwa na

Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (LIC)

Kwa kushirikiana na

Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT)

Na

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa
Agosti, 2018

SHUKRANI

Andiko hili linalofahamika kama*Mradi wa Uboreshaji wa Soko la Mbogamboga na Matunda la Kibaigwa* nimuendelezo wa maandiko kuhusu miradi ya mifano ambayo ipo chini ya ALAT kwa ufadhili wa LIC.

Katika mradi huu, Halmshauri iliamua kuboresha eneo la soko kwa lengo la kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na kuongeza kipato cha wananchi na Halmashauri kwa jumla.

Ninapenda kutumia nafasi hii kuushukuru Ubalozi wa Denmark kwa msaada wao wa fedha kupitia mradi wa LIC ambao umewezesha kupatikana fedha za kuandaa na kuchapisha andiko hili.

Tunatoa shukrani za kipekee kwa mratibu wa mradi wa LIC, Bw. Flemming Winther Olsen na timu yake kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa mradi huu kwa kushirikiana na washikadau wa kitaifa kama vile Ofisi ya Waziri Mkuu, OR-TAMISEMI, TNBC, TPSF na TCCIA.

Pia, tunatoa shukrani kwa uongozi wa mkoa wa Dodoma, uongozi wa Halmshauri ya Wilaya ya Kongwa, wafanyabiashara, wakulima na viongozi wote wa Mamlaka ya Mji Mdogo Kibaigwa kwa kutupatia taarifa zilizosaidia kukamilika kwa andiko hili.

Mwisho, ninapenda kutoa shukrani zangu kwa ALAT na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI hasa Bi. Husna A. Kandoro, Vicent Chomola na Anicetus Mramba kwa ukusanyaji wa taarifa zilizosaidia kupatiakana kwa andiko hili.

Abdallah S. Ngodu

Kaimu Katibu Mkuu– ALAT

ORODHA YA VIFUPISHO

ALAT	Association of Local Authorities of Tanzania
DC	District Council
KDC	Kongwa District Council
KTA	Kibaigwa Township Authority
LGA	Local Government Authorities
LIC	Local Investment Climate
PO – RALG	President's Office Regional Administration and Local Government
TBS	Tanzania Bureaus of Standards
TCCIA	Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture
TNBC	Tanzania National Business Council
TPSF	Tanzania Private Sector Foundation
VETA	Vocational Educational and Training Authority

YALIYOMO

SHUKRANI *3*

ORODHA YA VIFUPISHO *4*

YALIYOMO *5*

SURA YA KWANZA *6*

UTANGULIZI *6*

1.0 Usuli *6*

1.1 Ufafanuzi Kuhusu Mradi *7*

SURA YA PILI *8*

UFUMBUZI WA TATIZO *8*

2.0 Utangulizi *8*

2.1 Malengo ya Mradi *8*

2.2 Utekelezaji wa Mradi *9*

2.3 Gharama za Utekelezaji wa Mradi *11*

SURA YA TATU *13*

MAFANIKIO, CHANAGAMOTO, VIKWAZO, UIMARA, NA MAFUNZO KUTOKA KATIKA MRADI *13*

3.0 Mafanikio ya Mradi *13*

3.1 Mafunzo Kutoka katika Mradi *14*

3.2 Mipango ya Uimarishaji wa Soko *14*

3.3 Changamoto *14*

SURA YA NNE *15*

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO *15*

4.0 Hitimisho *15*

4.1 Mapendekezo *15*

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ni moja kati ya Halmashauri saba (7) zinazounda mkoa wa Dodoma. Halmashauri zingine ni pamoja na Chamwino, Kondoa, Mpwapwa, Chemba na Jiji la Dodoma. Chamwino ipo katika latitudo 5° 30- 6° Kusini na longitudo 36° 15° – 36 Magharibi mwa Griniwichi. Kwa upande wa mwinuko, eneo hili lipo baina ya mita 900 na 100 kutoka usawa wa bahari. Mji wa Kongwa ndiyo makao makuu ya wilaya hii na upo umbali wa km 86 kutoka jiji la Dodoma.

Kwa upande wa mipaka, Halmashauri ya Kongwa inapakana na Halmashauri ya Wilaya yaChamwino kwa upande Magharibi, Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto (mkoa wa Manyara) kwa upande wa Kaskazini, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa (mkoa wa Morogoro) kwa upande wa Magharibi na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa kwa upande wa Kusini.

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina tarafa tatu ambazo ni Mlali, Kongwa na Zoissa. Pia, ina kata 22, vijiji 74 na vitongoji 312. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina jumla ya wakazi 318,995, kati yao, watu 156,982 ni wanaume na watu 162, 013 ni wanawake. Ongezeko la watu kwa mwaka ni wastani wa asilimia 2.4.

Kwa asili, mazao (ya chakula na biashara) yanayostawi katika eneo hili ni pamoja na mahindi, mtama, karanga, mihogo, alizeti, maharage, mbogamboga (hasa kandokando ya mito iliyopo katika vijiji vya Tubugwe na Chamkoroma).

Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ina maeneo ya miji/senta kama vile Kongwa, Mlali, Mkoka, Pandambilli, Mbande, Hembahemba na Kibaigwa. Mji wa Kibaigwa ni sehemu maarufu sana kwa sababu ya kuwepo kwa soko la kimataifa la mahindi kwa ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika.

1.1 Ufafanuzi Kuhusu Mradi

Mnamo Novemba 20,2014 LIC ilianza rasmi miradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa baada ya kukamilika kwa andiko mradi lililolenga kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali. Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa iliandaa maandiko ya miradi yapatayo 21 na kuyawasilisha kwa LIC kwa ajili ya kuyapitisha. Kati ya maandiko hayo, miradi 7 ilifanikiwa kupata fedha kutoka LIC.

Miradi iliyofanikiwa kupata pesa kutoka LIC ni pamoja na Mradi wa Kituo Maalumu cha Biashara (*One Stop Business Centre* (OsBC), Mradi wa Soko la Mbogamboga Kibaigwa, Mradi wa Utunzaji wa Kumbukumbu/Kanzi Data, Mradi wa Ufugaji Kuku wa Kongwa na Mbande, Mradi wa Kituo cha Biashara ya Alizeti Pandambili, Mradi wa Ujenzi wa Soko la Biashara Mkoka, na Mradi wa Uboreshaji wa Mnada wa Mbande.

Kielelezo Na. 1: Picha ya kushoto ni jengo la soko kama linavyoonekana kutokea nje na picha ya kulia ni wauzaji wa bidhaa za mbogamboga pamoja na wateja wao katika soko la mbogamboga la Kibaigwa.

SURA YA PILI

UFUMBUZI WA TATIZO

2.0 Utangulizi

Kabla ya LIC kuanza kulifufua soko la mbogamboga la Kibaigwa, wafanyabiashara wa mbogamboga na matunda hawakuwa na sehemu ya uhakika ya kuuzia bidhaa zao. Hivyo basi, baada ya LIC kuanza juhudi hizi ziliisaidia sana Halmashauri kuimarisha soko la kuuzia bidhaa za mbogamboga na matunda kwa kuwapatia sehemu nzuri ya kufanyia biashara zao.

Huko nyuma soko hili lilikabiliwa na changamoto nyingi kama vile upotevu wa mapato ya ushuru, ukosefu wa maji safi, kukosekana kwa mifumo ya maji taka, ukosefu wa vyoo, mrundikano wa taka na ukosefu wa umeme wa uhakika. Kupitia msaada wa LIC matatizo haya yamepatiwa ufumbuzi kwa zaidi ya 80%.

2.1 Malengo ya Mradi

Baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kubaini changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wa mbogamboga na matunda wa Kibaigwa, waliamua kuandaa andiko la mradi ili kuboresha hali hii. Lengo lilikuwa ni kuwakusanya wafanyabiashara wote wa mbogamboga katika eneo moja na kurahisisha zoezi la ukusanyaji kodi kwa Halmashauri.

Kabla ya kuanza shughuli za ujenzi wa soko, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa iliunda kikosikazi maalumu. Timu hii ililenga kusimamia kazi zote za mradi zinazohusiana na uboreshaji wa soko kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kikosikazi kilijumuisha wajumbe sita, kati ya hao, wajumbe watatu kutoka sekta binafsi (uongozi wa wafanyabiashara ya mbogamboga na matunda) na wajumbe watatu kutoka serikalini. Kwa jumla, mradi huu ulilenga kufanya ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi (PPP).

Kikosikazi kilijumuisha watu wafuatao: Idd Mwajanga– Mwenyekiti (sekta binafsi), Athuman Nzenga– Katibu (serikali), Mapenzi Mchuzi– Mhasibu (sekta binafsi), Juma Mukhaimar– Mjumbe (serikali), Twayibu Hussein– Mjumbe (sekta binafsi) na Paschal Mushi– Mjumbe (serikali).

Timu hii ilifanya kazi usiku na mchana kuhakikisha kuwa mradi unakamilika ndani ya muda uliopangwa. Aidha, timu hii ilihusika na majukumu yote ya mradi ikiwemo usimamizi, ufuatiliaji na usimamizi wa fedha za ujenzi.

Kielelezo Na. 2: Picha ya jengo la soko likiwa limegawanywa katika vizimba ambavyo hutumika kwa biashara ya mbogamboga.

2.2 Utekelezaji wa Mradi

Kataika utekelezaji wa mradi huu, LIC ilitoa fedha katika awamu tatu. Katika awamu ya kwanza, mradi ulipokea kiasi cha Tsh. 39,782,800/=. Fedha hizi zilitolewa mwezi Novemba, 2015. Fedha hizi zilitumika katika kufanya matengenezo ya jengo la banda la mchele, kufanya marekebisho ya mifumo ya maji safi na majitaka, ujenzi wa sehemu ya kuhifadhi taka na ujenzi wa banda la kufanyia biashara. Awamu hii ilikamilika rasmi mwezi Machi, 2017 ambapo jumla ya Tsh.39,782,720.00/= zilitumika.

Kielelezo Na. 3: Picha ya juu ni banda la mchele na picha ya chini ni sehemu maalumu ya kuhifadhia taka.

Awamu ya pili ya mradi ilianza mwezi Mei, 2016 na kumalizika mwezi Septemba, 2016. Kazi zilizofanyika katika awamu hii ni pamoja na ujenzi wa banda la biashara, choo, mifumo ya majitaka, sehemu ya kuhifadhi taka. Pia, fedha zilitumika kufanya maboresho katika banda la kuuzia samaki na matunda. Jumla ya Tsh.50,225,300.00/=zilitumika katika awamu hii.

Kielelezo Na. 4: Picha ya kushoto ni vizimba vya kuuzia samaki na kulia ni jengo la choo.

Katika awamu ya tatu, mradi ulipokea jumla ya Tsh.76,817,134.24/=. Fedha hizi zilitumika katika ujenzi wa vyoo, mifumo ya majitaka, sehemu maalumu ya kuhifadhi taka na mfumo ya umeme. Baadhi ya fedha zilizobaki zilitumika kujenga vizimba 27 ambavyo hutumika kuuzia bidhaa mchanganyiko. Pia, fedha nyingine zilitumika kurekebisha mifumo ya majitaka, kumalizia jengo la umeme wa dharura na kumalizia banda la kuuzia nyanya. Vilevile, zipo fedha zilizohidhiwa kwa ajili ya dharura (uangalizi wa mradi kwa kipindi cha miezi sita).

Kielelezo Na. 5: Picha ya kushoto ni banda la nyanya na picha ya kulia ni sehemu maalumu ya kuhifadhia taka.

2.3 Gharama za Utekelezaji wa Mradi

Jumla ya Tsh. 166,825,154.24/= zilitumika katika matengenezo ya soko la matunda na mbogamboga la Kibaigwa. Sehemu kubwa ya fedha hizi zilifadhiliwa na LIC isipokuwa eneo la ujenzi, majengo 4 ambayo yalikuwa hayakamilika na kiasi cha Tsh mil 304 za fidia katika eneo la mradi. Ujenzi ulifanywa na mafundi wa kawaida kutoka katika eneo la mradi. Kwa jumla, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kibaigwa walitangaza zabuni ya ujenzi ambapo mafundi walitakiwa kuomba kandarasi ya ujenzi. Zoezi hili liliendeshwa na ofisi ya mhandisi wa wilaya pamoja na kamati ya ujenzi ya wilaya. Mafundi walioshinda zabuni walikuwa wakilipwa fedha za ujenzi tu. Aidha, kamati ya ujenzi ilikuwa na jukumu la kununua vifaa vyote vya ujenzi.

SURA YA TATU

MAFANIKIO, CHANGAMOTO, VIKWAZO, UIMARA, NA MAFUNZO KUTOKA KATIKA MRADI

3.0 Mafanikio ya Mradi

Kupitia mradi huu wa ujenzi wa soko la mbogamboga na matunda,Mamlaka ya Mji imepata mafanikio yafutayo:

1. Kuongezekakwa makusanyo ya Mji Mdogo wa Kibaigwa. Taarifa zinaonesha kuwa, kabla ya mradi huu kukamilika (Novemba, 2015) kulikuwa na makusanyo ya Tsh. 900,000/= kwa mwezi na baada ya mradi kukamilika (Julai, 2016) makusanyo yaliongezeka na kufikia Tsh. 1,700,000/= kwa mwezi.

2. Soko hili limewavutia wawekezaji mbalimbali kama vile Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi Wenye Maghala (*WAREHOUSE RECEIPTS REGULATORY BOARD*).Aidha, TANESCO walivutika na kuunganisha umeme katika soko. Mamlaka ya Maji Safi Kibaigwa imesambaza maji katika eneo la soko na maeneo yanayozunguka soko. Maduka zaidi ya 16 yamejengwa jirani na eneo la soko.

3. Soko limetoa fursa kwa wafanyabiashara zaidi ya 400 (wanawake 250 na wanaume 150) kwa kuwapatia mahali pa uhakika kwa ajili ya kuuzia na kununulia biashara zao. Hali hii imechochea ongezeko la uzalishaji wa mbogamboga na matunda ndani na nje ya Halmashauri na kuongeza kipato cha wananchi hasa vijana na wanawake.

4. Soko limechangia ongezeko kubwa la mapato ya Mji Mdogo wa Kibagwa kutoka Tsh. 12,408,000/= hadi Tsh. 86,184,000/=.

3.1 Mafunzo Kutoka katika Mradi

1. Ushirikiano baina ya sekta binafsi na serikali (PPP) ulikuwa na nguzo muhimu katika kuusimamia mradi;
2. Kuwapo kwa usimamizi madhubuti wa mradi na ushirikishwaji wa taasisi binafsi kulisaidia sana katika utekelezaji mzuri wa mradi; na
3. Soko la mbogamboga na matunda la Kibaigwa linafanya vizuri kwa kuwa kuna usimamizi imara kutoka katika Mamlaka ya Mji na jumuiya ya wafanyabiashara waliopo ndani ya soko husika.

3.2 Mipango ya Uimarishaji wa Soko

Ili kuimarisha mradi huu, soko lina mipango ifuatayo:

1. Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kufanyia biashara zao katika eneo la soko; na
2. Kupitia jumuiya ya wafanyabiashara waliopo ndani ya soko wanaendelea kukusanya michango kutoka kwa wanachama wao kwa ajili ya kuimarisha hali ya usafi na ulinzi katika eneo la soko.

3.3 Changamoto

Soko linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Bado wapo wafanyabiashara wengi wanaofanya shughuli zao nje ya eneo la soko hivyo kuikosesha Mamlaka ya Mji mapato yake;
2. Uanzishwaji wa masoko bubu/yasiyo rasmi katika maeneo mbalimbali ya Mamlaka ya Mji; na
3. Kupishana kauli kwa vingozi wa Halmashauri na wale wa serikali kuu kuhusu kadhia ya ufanyaji biashara katika maeneo/masoko yasiyo rasmi ndani ya Mamlaka ya Mji.

SURA YA NNE

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

4.0 Hitimisho

Kuwepo kwa soko la kisasa kwa ajili ya uuzaji wa mazo ya mbogamboga na matunda kumesaidia sana ongezeko la mapato kwa Mamlaka ya Mji na kuinua hali za kiuchumi kwa jamii inayolizunguka soko husika. Aidha, mradi wa soko umevutia huduma mbalimbali muhimu kulizunguka eneo la soko, hivyo kuboresha kipato na ustawi wa wafanyabiashara kwa jumla.

Pia, kuwepo kwa uongozi imara wa wafanyabiashara umefanikisha kuundwa kwa kanuni na sheria mbalimbali zenye lengo la kulinda miundombinu ya soko na kuimarisha hali ya usafi katika eneo lote la soko. Ni wazi kuwa viongozi na wanachama wao wanaofanya biashara katika soko hili wanafahamu fika kuwa miundombinu ya soko hili inapaswa kulindwa kwa manufaa ya kizazi hiki na kizazi kijacho.

4.1 Mapendekezo

Yafuatayo ni mapendekezo muhimu kwa ajili ya kuimarisha mradi huu:

1. Mamlaka ya Mji inapaswa kuimarisha sheria zake ndogondogo kwa lengo la kukabiliana na watu wanaoharibu miundombinu ya soko; na
2. Maoni kutoka kwa wadau mbalimbali yenye lengo la kujenga ni muhimu yakasikilizwa na kufanyiwa kazi.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na:

Katibu Mkuu Mtendaji wa ALAT

S. L. P. 2049

Simu: +255 784 514 245

Dodoma, Tanzania

Barua pepe: info@alat.or.tz

Tovuti: www.alat.or.tz